**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO MIFUGO NA UVUVI**

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA**

# MWONGOZO WA UTOAJI LESENI KWA VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS)


*Mrajis wa Vyama vya Ushirika,*
*S.L.P 201,*
***DODOMA.***

*Barua pepe: ushirika@ushirika.go.tz*
*Tovuti: www.ushirika.go.tz*


***July, 2017***

# YALIYOMO

**VIFUPISHO** ........ iii

**DIBAJI** ........ iv

**SHUKRANI** ........ vi

**1.0 UTANGULIZI** ........ 1

*1.1 CHIMBUKO LA MWONGOZO* ........ 2

*1.2 DHANA YA UTOAJI WA LESENI* ........ 3

*1.3 MADHUMUNI YA UTOAJI WA LESENI* ........ 3

**2.0 MASHARTI YA KUOMBA LESENI** ........ 4

*2.1 SABABU ZA SACCOS KUOMBA LESENI* ........ 5

**3.0 BIDHAA NA HUDUMA ZINAZOWEZA KUTOLEWA NA SACCOS ZENYE LESENI** ........ 5

*3.1 BIDHAA NA HUDUMA AMBAZO HAZITATOLEWA NA SACCOS ZENYE LESENI ISIPOKUWA KWA IDHINI YA MRAJIS* ........ 5

**4.0 UTOAJI WA LESENI** ........ 6

*4.1 UKAGUZI WA CHAMA;* ........ 6

*4.2 UTOAJI LESENI KWA MASHARTI* ........ 6

*4.3 SACCOS KUKATALIWA KUPEWA LESENI* ........ 6

4.2.1 SABABU ZA SACCOS KUKATALIWA MAOMBI YA LESENI ........ 7

**5 .0 SIFA NA TARATIBU ZA CHAMA KUFUNGUA MATAWI** ........ 7

5.1 KUBADILISHA ENEO LA BIASHARA ........ 8

5.2 SHUGHULI ZA UWAKALA AU HUDUMA NYINGINEZO ........ 8

5.3 MAHITAJI YA UENDESHAJI WA CHAMA ........ 8

**6.0 MIKOPO SHIRIKISHI (*Loan participation*)** ........ 9

**7.0 USIMAMIZI WA KISHERIA** ........ 10

**8.0 UDHIBITI WA MENEJA MSIMAMIZI** ........ 11

8.1 MAJUKUMU NA MAMLAKA YA MENEJA MSIMAMIZI ........ 11

**9.0 KUSITISHWA KWA MALIPO YA FIDIA YA USIMAMIZI WA KISHERIA** .................. 11

**10. HITIMISHO** .................. 12

***VIAMBATISHO:*** .................. 13

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| SACCOS | Savings and Credit Co-operative Society |
| FICOS | Financial Instituion Cooperative Society |
| MIVARF | Marketing Infrastructure Value Addition and Rural Financing |
| SCCULT | Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania |
| MoCU | Moshi Cooperatives University |

## DIBAJI

Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ni miongoni mwa aina ya Vyama vya Ushirika ambavyo vilianza kushamiri mwanzoni mwa miaka ya 1960. Vyama hivi vimekuwa vikisajiliwa na kusimamiwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika iliyokuwepo kwa wakati huo ambazo zilipitia katika mabadiliko mbalimbali. Vyama hivyo vilikuwa vikisajiliwa na kusimamiwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika chini ya Idara ya Maendeleo ya Ushirika ambayo ilikuwa ikiwajibika chini ya Wizara iliyokuwa na dhamana ya Ushirika.

Vyama vya ushirika wa Akiba na Mikopo vimekuwa vikiongezeka kwa kasi katika maeneo ya mijini na vijijini na kukusanya Akiba, Amana, Hisa na utoaji wa mikopo mikubwa pasipo kuzingatia taratibu za taasisi za fedha pamoja na viwango vya ubora katika uendeshaji wake. Hali hii imesababisha fedha za wanachama wa SACCOS kuwa kwenye hatari ya kupotea ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuathiri sekta ya kifedha nchini. Sheria za Vyama vya Ushirika zilizokuwepo awali pamoja na Sheria ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2004 hazikuweza kuanisha maeneo ya kusimamia SACCOS hizo kwa ukamilifu.

Usimamizi wa SACCOS, umekuwa na changamoto mbalimbali ambazo zimedhoofisha maendeleo yake, zikiwemo kutokuwepo na usimamizi wakutosha, kutokuwepo na miongozo stahiki kwa ajili ya usimamizi, wajumbe wa bodi na watendaji kutokuwa na sifa na weledi wa uongozi na usimamizi wa SACCOS. Aidha, SACCOS bila kuzingatia ukubwa wake zilikuwa zinatoa huduma/bidhaa mbalimbali na kufungua matawi au kufanya shughuli za uwakala na mikopo shirikishi ambapo baadhi ya SACCOS hizo hazikuwa na uwezo wa kuzisimamia ipasavyo.

Katika kuimarisha usimamizi wa SACCOS, Serikali imekuwa ikuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na Benki Kuu kutunga Kanuni za FICOS za mwaka 2005 kwa ajili ya kuzipatia leseni na kuzisimamia SACCOS zenye mtaji uliozidi shilingi milioni mia nane (Tzs 800,000,000) pamoja na jitihada hizo, hakuna SACCOS iliyowahi kupatiwa leseni kutoka na na mkanganyiko wa baadhi ya vipengele ikiwa ni pamoja na mtaji na umiliki wa hisa kati ya kanuni ya Vyama vya Ushirika na Kanuni za FICOS. Aidha SACCOS zilizokuwa na sifa hazikuwa tayari kuomba leseni na kusimamiwa na Benki Kuu.

Ili kuweza kuhakikisha kuwa SACCOS hizi kubwa zinakuwa na usimamizi wa karibu kwania ya kulinda fedha za wanachama (risk based supervision) ilionekana kuna haja ya kuziangalia kwa undani na kutoa maoni juu ya usimamizi wake.

Kutokana na mabadiriko ya sekta za fedha na umuhimu wake nchini, ilionekena kuwa ipo haja ya kuimarisha usimamizi wa SACCOS. Ili kuhakikisha kuwa SACCOS zinasimamiwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika utafiti ulifanyika na Washauri waelekezi walipendekeza kuwa iko haja ya kuwa na Kanuni maalumu ya kusimamia SACCOS na kuzigawa katika Makundi mawili ili kuimarisha usimamizi.

Kwa kuzingatia changamoto hizo, pamoja na mambo mengine Serikali ilitunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ambayo imesababisha kutungwa kwa Kanuni maalum kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa SACCOS. Kanuni hizo zinampa mamlaka Mrajis kusajili na kusimamia SACCOS na kuziweka katika makundi mawili tofauti ambayo ni SACCOS zisizo na Leseni na SACCOS zenyeLeseni.

Mrajis ameandaa muongozo huu unaoainisha utaratibu, vigezo na masharti ya utoaji wa leseni kwa SACCOS kwa kuzingatia Kanuni za SACCOS. Aidha mwongozo huu utawezesha uimarishaji wa uendeshaji na usimamizi wa SACCOS zitakazopatiwa Leseni.

TITO B. HAULE

**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

Julai, 2017

## SHUKRANI

Kwa niaba ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwanjia moja ama nyingine kwa walioshiriki katika maandalizi ya Mwongozo huu. Shukrani zangu ziwaendee, Progarmu ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF), ambao wamefadhili muongozo huu, *Financial Sector Programme* (FSP), Mtaalamu mwelekezi kutoka Baraza la Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo Duniani *(WOCCU)*, waliowezesha kuandaa rasmu ya muongozo huu; Watalamu kutoka Benki Kuu ya Tanzania (B.o.T), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SCCULT), Wataalamu kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na wengine kwa namna moja ama nyingine wamefanikisha kukamilika kwa mwongozo huu.

## 1.0 UTANGULIZI

Taasisi ndogo za kifedha kwa sehemu kubwa nchini zinaundwa na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo-*Savings and Credit Coopaertive society* (SACCOS). Wananchi wengi wamekuwa na imani na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo na kuendelea kuvitumia kama njia muafaka ya kukidhi mahitaji yao ya kifedha na kijamii katika maeneo ya mjini na vijijini hususan vijijini. Kundi kubwa la wananchi wanaojiunga na 'SACCOS' ni la wenye vipato vya kati na chini ambalo limeweka matarajio makubwa katika vyama hivi. Mbali na changamoto ya soko huria, ushindani mkubwa katika biashara ya fedha pamoja na mtikisiko wa uchumi uliozikabili taasisi nyingi za kifedha Duniani, bado 'SACCOS' zimeendelea kuwepo na kukidhi mahitaji ya wanachama wake. Hata hivyo, SACCOS zinatakiwa kuboresha uendeshaji na usimamizi wa shughuli zake ili ziweze kushindana na taasisi nyingine za kifedha katika kutoa huduma zilizo bora na kwa wakati kwa wanachama wake.

Aidha, SACCOS nyingi nchini zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mitaji midogo, idadi ndogo ya wanachama, uwekezaji mdogo katika hisa, Akiba na mikopo, uandishi na utunzaji usioridhisha wa hesabu na kumbukumbu za Vyama, ukosefu wa viongozi na watendaji wenye weledi, ubunifu na uaminifu, ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Sera, miongozo na Masharti ya Vyama. Pia SACCOS zimeshindwa kuweka matengo na uwepo wa mikopo isiyorejesheshwa pamoja na kutotumia mifumo mizuri ya kumbukumbu ikiwamo TEHAMA.

Matokeo ya changamoto hizi yanatishia uhai na maendeleo endelevu ya Vyama na sekta nzima ya fedha nchini. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013, Kifungu cha 141(1) na (3) imeandaa Kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) za Mwaka 2014 kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa Vyama vya Ushirika nchini. Kanuni hizo za SACCOS zimejielekeza katika kuimarisha Uendeshaji na Usimamizi wa SACCOS na kuboresha shughuli zake kwa kuzingatia maeneo hatarishi Kanuni za SACCOS zinaondoa usimamizi wa SACCOS katika mamlaka mbili tofauti zilizokuwepo mwanzoni (Benki Kuu ya Tanzania na Mrajis wa Vyama vya Ushirika) na kuweka usimamizi wake katika mamlaka moja ambayo ni Tume ya maendeleo ya ushirika. Aidha, kanuni hizi zinafuta Kanuni mbili zilizokuwepo ambazo ni Kanuni ya Vyama vyote vya Ushirika ya Mwaka 2004 (SACCOS zikiwemo) na Kanuni za taasisi za Kifedha za mwaka 2005

(FICOs regulations) iliyokuwa inasimamia SACCOS kubwa zenye mtaji wa zaidi ya Sh milioni mia nane (Milioni 800).

Kanuni zimeainisha makundi mawili ya SACCOS kulingana na ukubwa na uwezo wake kimtaji, uongozi na aina ya huduma zitolewazo na Vyama husika. Makundi hayo ni SACCOS zilizosajiliwa na SACCOS zenye leseni.

Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika ndiyo yenye mamlaka ya kutoa leseni kwa SACCOS zenye sifa na vigezo, na itatoa Leseni kwa SACCOS zilizosajiliwa na ambazo zitakuwa na mtaji, zinazotaka kutoa huduma/ bidhaa za ziada, zinazotaka kufungua matawi, na zinazotaka kutoa mikopo shirikishi, mahitaji makubwa ya mikopo, eneo kubwa la uendeshaji wa shughuli za chama pamoja na weledi wa viongozi na menejimenti ya chama. Vyama vitakavyopewa leseni vitahitaji utaalam zaidi katika usimamizi na udhibiti wa shughuli za Vyama hivyo kutokana na hatari zinazovikabili katika uendeshaji wa shughuli zake. Kutokana na umuhimu huo, Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika imeandaa mwongozo utakaowezesha SACCOS na wadau mbalimbali kujua vigezo, Masharti, taratibu nzima za uombaji, utoaji wa leseni na uendeshaji wa SACCOS zenyewe. Aidha, mwongozo huu utatumika katika usimamizi na tathmini ya uendeshaji wa SACCOS zenye leseni pamoja na uwasilishaji wa taarifa zake.

Ofisi ya Mrajis inatarajia kwamba, utoaji wa leseni kwa vyama vitakavyokidhi matakwa ya Sheria na Kanuni, utarasimisha shughuli na bidhaa zitolewazo na Vyama hivyo na chama hakitaweza kutoa huduma/bidhaa iliyo juu ya uwezo wake na kasi ya ukuaji wa 'SACCOS' itashabihiana na matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za Ushirika. Matokeo ya utoaji wa leseni yataongeza ufanisi katika usimamizi wa SACCOS, utoaji huduma kwa wanachama na upatikaji wa takwimu za SACCOS. Hii itaongeza imani kwa wananchi katika kutumia huduma za SACCOS na kuchangia kipato cha nchi.

## 1.1 CHIMBUKO LA MWONGOZO

Tangu Mwaka 2003 kulionekana kuwepo na umuhimu wa uimarishaji wa usimamizi na uendeshaji wa shughuli za SACCOS nchini. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kuwa SACCOS zinaendeshwa na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria, taratibu na misingi bora ya uendeshaji wa taasisi za kifedha (best practices in financial sectors). Mwaka 2004 ilitungwa Kanuni ya vyama vya ushirika ambayo ilikuwa na maeneo mahususi katika uendeshaji na usimamizi wa SACCOS (Kanuni 75-106). Aidha, ilionekana kuwa baadhi ya SACCOS ziliendelea kukua na

kupanua shughuli zake na kujiendesha kama benki na hivyo Serikali ilitunga Kanuni mwaka 2005 (FICOs regulations) ambazo zililenga kusimamia utoaji wa leseni na usimamizi wa SACCOS zenye mtaji uliozidi Shilingi milioni mia nane.

SACCOS hizo zilitakiwa kupewa leseni na kusimamiwa na Benki kuu ya Tanzania (BOT). Hata hivyo tangu mwaka 2005 hakuna SACCOS iliyoomba na kupatiwa leseni kutokana na kukinzana kwa baadhi ya vipengele vya Kanuni tajwa hapo juu na kutokuwepo kwa utayari na utashi wa SACCCOS.

Katika kuondoa mapungufu hayo, Serikali ilitunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 ambayo imesababisha kutungwa kwa Kanuni za vyama Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS). Kanuni hizi zimeanisha matakwa ya utoaji wa leseni katika SACCOS. Ili kutekeleza matakwa hayo, ofisi ya Mrajis imeandaa muongozo unaoelezea utaraibu mzima wa utoaji wa leseni katika SACCOS na usimamizi wake.

## 1.2 DHANA YA UTOAJI WA LESENI

Utoaji wa leseni kwa SACCOS ni hatua ambayo SACCOS inaomba na kupewa leseni kwa ajili ya kutoa bidhaa na huduma zilizoainishwa katika Kanuni za SACCOS. Aidha, Leseni hiyo huongeza wigo wa shughuli za chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo katika kutoa bidhaa/huduma za ziada za kifedha kwa wanachama wake tofauti na SACCOS ndogo (Registered SACCOS). Utoaji wa leseni katika SACCOS unalenga kuimarisha ufanisi katika utendaji na usimamizi wa shughuli za SACCOS hizo na kupunguza hatari zinazoweza kuzikumba.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTOAJI WA LESENI

SACCOS zenye leseni zitaweza kuongeza wigo wa kuendesha shughuli zake kwa kutoa hoodlum mbalimbali zaidi ya zile zilizotakuwa zinatolewa kabla ya kupewa leseni.. Aidha, SACCOS zitakuwa na uwezo wa kufungua matawi pamoja na milango ya huduma katika maeneo mbalimbali pamoja na kutoa mikopo shirikishi (kukopeshana).

Aidha, Vyama vyenye leseni vitatakiwa kujiendesha kwa weledi Zaidi na kusimamiwa na viongozi na watendaji wenye sifa , ambao watasaidia kubuni bidhaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya kukidhi matakwa ya wanachama wake. Uwepo wa miongozo, mifumo na usmamizi imara utapunguza hatari kwa wanachama kupoteza fedha zao walizowekeza katika SACCOS. Vilevile, SACCOS zenye leseni zitaweza kusimamiwa kwa ukaribu na Maafisa Ushirika ambao watatoa ushauri wa kitaalamu katika kuendesha shughuli zao. AidhaSACCOS zinatakiwa kuandaa mpango

mkakati wa biashara pamoja na kutumia mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa taarifa kwa Mrajis.

## 2.0 MASHARTI YA KUOMBA LESENI

Chama chochote cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kilichosajiliwa na ambacho kinataka kutoa bidhaa na huduma za ziada tofauti na zilizoainishwa katika usajili wake, kitatakiwa kuomba leseni. Aidha, ili chama hicho kiweze kupewa leseni lazima kikidhi masharti yaliyoainishwa katika kanuni za SACCOS ambayo ni pamoja na yafuatayo.

i. SACCOS iwe na mtaji tete (Core Capital) usiopungua milioni mia moja.

ii. Kulipa ada ya maombi ya Leseni kama itakavyoelekezwa na Mrajis.

iii. Barua ya maombi kwa kuzingatia mfumo (format) maalum kama ilivyoelekezwa katika Fomu Na.1 ya Jedwali la Kwanza

iv. Majina na anwani kamili za wajumbe wa Bodi, Kamati ya usimamizi na maafisa waandamizi wa chama.

v. Wasifu binafsi wa wajumbe wa Bodi, Kamati ya usimamizi na Maafisa waandamizi wa chama.

vi. Bakaa za hisa na mikopo ya kila mjumbe wa Bodi, kamati ya usimamizi na Maafisa waandamizi.

vii. Nakala iliyothibitishwa kisheria ya Masharti ya chama inayokidhi vigezo vya kupewa leseni.

viii. Hati ya usajili wa chama.

ix. Nakala za Sera za mikopo, Uwekezaji, Rasilimali watu, Akiba, Ukwasi, Fedha, Makusanyo na Taratibu za udhibiti wa ndani

x. Uthibitisho wa vifaa vya kutunzia fedha vyenye usalama na ulinzi wa kutosha na uwepo wa bima ya fedha hizo.

xi. Uthibitisho wa angalau Wajumbe wawili wa Bodi na Mjumbe mmoja wa Kamati ya Usimamizi na Menejimenti wenye uzoefu katika taaluma ya uhasibu, ukaguzi, utawala, fedha, uchumi au uongozi. Pia, Meneja Mkuu awe na uzoefu wa angalau miaka miwili katika uendeshaji wa shughuli za SACCOS au taasisi nyingine ya fedha.

xii. Nakala ya mpango mkakati wa miaka mitatu ikijumuisha dhima, muundo wa Utawala, bidhaa na huduma, mipango ya upanuzi wa tawi, mkakati wa ukuaji, makisio ya Mapato na Matumizi, Mizania, mtiririko wa fedha na vigezo vilivyotumika kufanya makisiso hayo.

xiii. Nakala za taarifa ya ukaguzi wa hesabu kwa miaka miwili iliyopita.

xiv. Muhtasari wa Mkutano Mkuu uliyoidhinisha maombi ya leseni.

xv. Nakala ya uthibitisho wa ajira ya Mkaguzi wa Ndani au Mkataba wa mtoa huduma ya Mkaguzi wa Ndani.

xvi. Uthibitisho wa uwepo wa mfumo wa TEHAMA ambao utaweza:-

- Kutoa taarifa za mwezi kuhusu Mapato na matumizi, Mizania, mikopo iliyocheleweshwa na umri wa mikopo.
- Kukidhi matakwa ya Kisheria ya utoaji wa taarifa ya kila mwezi.
- Kutoa utaratibu na maelezo kwa ajili ya miamala ya ziada inayohusu bidhaa na huduma mpya zitakazotolewa.

## 2.1 SABABU ZA SACCOS KUOMBA LESENI

SACCOS inaweza kuomba Leseni endapo:-

i. Inataka kutoa bidhaa au huduma zaidi ya zilizoruhusiwa katika usajili wake.

ii. Inataka kufungua matawi ya utoaji huduma na bidhaa.

iii. Inataka kuwa wakala au milango ya huduma.

iv. Inataka kutoa mikopo shirikishi kwa vyama vingine.

v. Imekuwa na idadi kubwa ya wanachama katika maeneo mbalimbali (Outreach member penetration).

vi. Pamoja na sababu nyingine zitakazoelekezwa na Mrajis kadri atakavyoona inafaa.

## 3.0 BIDHAA NA HUDUMA ZINAZOWEZA KUTOLEWA NA SACCOS ZENYE LESENI

i. Hisa za lazima na hiari za Wanachama.

ii. Akiba na Amana.

iii. Mikopo kwa wanachama.

iv. Mikopo shirikishi.

v. Bidhaa na huduma nyingine baada ya kupata idhini ya Mrajis.

## 3.1 BIDHAA NA HUDUMA AMBAZO HAZITATOLEWA NA SACCOS ZENYE LESENI ISIPOKUWA KWA IDHINI YA MRAJIS

i. Uendeshaji wa akaunti ya hundi;

ii. Ubadilishaji wa fedha za kigeni;

iii. Biashara za nje ya nchi;

iv. Shughuli za udhamini;

v. Utumaji wa fedha;
vi. Kadi za kuweka na kutoa fedha;
vii. Malipo ya maagizo na uhamishaji wa fedha;
viii. Vituo vya mauzo;
ix. Kuwekeza katika mitaji;
x. Kununua au kujipatia mali za kudumu na zisizozalisha zenye thamani ya zaidi ya matakwa ya kisheria kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu;
xi. Shughuli yoyote tofauti na utoaji wa bidhaa na huduma za kifedha kwa wanachama wake; na
xii. Shughuli zingine kama itakavyoelekezwa na Mrajis.

## 4.0 UTOAJI WA LESENI

Mrajis wa Vyama vya Ushirika atatoa leseni kwa SACCOS ambazo zitakuwa zimekidhi matakwa na vigezo vilivyowekwa katika mwongozo huu. Endapo SACCOS itakuwa imekidhi vigezo hivyo, Mrajis ataipatia leseni ndani ya siku 60 kwa kutumia fomu namba 2.

Kabla ya kutoa leseni Mrajis atazingatia mambo yafuatayo:-

### 4.1 UKAGUZI WA CHAMA;

Ili kujirihisha na taarifa zilizowasilishwa na SACCOS wakati wa maombi ya leseni, Mrajis atafanya ukaguzi katika maeneo yafuatayo;-

i. Hali ya kifedha ya chama
ii. Miundombinu ya chama
iii. Sifa na weledi wa wajumbe wa bodi na maafisa waandamizi

### 4.2 UTOAJI LESENI KWA MASHARTI

Mrajis anaweza kutoa leseni ya masharti kwa SACCOS iliyosajiliwa kufanya shughuli zake kama SACCOS yenye leseni kwa muda maalum kama itakuwa haijakidhi baadhi ya masharti na vigezo ambavyo Mrajis anaamini kuwa SACCOS hiyo inaweza kuyakidhi ndani ya muda huo.

### 4.3 SACCOS KUKATALIWA KUPEWA LESENI

- Mrajis anaweza kukataa kutoa leseni kwa SACCOS yoyote iliyosajiliwa ambayo imeshindwa kutimiza masharti ya leseni kwa mujibu wa Kanuni na Mrajis ataitaarifu kwa maandishi SACCOS husika.

- SACCOS ambayo maombi yake yamekataliwa inaweza kutuma maombi mapya kwa kurekebisha mapungufu yaliyosababisha kukataliwa kupewa leseni na maombi hayo yatachukuliwa kama maombi mapya ya Leseni.
- SACCOS yoyote ambayo hajaridhishwa na uamuzi wa Mrajis wa kukataa kuipatia leseni anaweza kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ndani ya siku 60 kutoka tarehe ya kupokea notisi ya maandishi ya kukataliwa kupewa leseni na Waziri atafanya maamuzi ndani ya siku 30.

### 4.2.1 SABABU ZA SACCOS KUKATALIWA MAOMBI YA LESENI

SACCOS inaweza kukataliwa kupewa Leseni iwapo itashindwa kukidhi vigezo vilivyowekwa kwenye Kanuni za SACCOS. Zifuatazo ni sababu za kukataliwa kwa maombi ya leseni.

a) Kushindwa kukidhi masharti ya maombi ya leseni
b) Iwapo SACCOS iliyosajiliwa haiwezi kujiendesha kiuchumi; na
c) Sababu nyingine yoyote kwa maoni ya Mrajis na ambayo inapaswa kuzingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za SACCOS.

## 5 .0 SIFA NA TARATIBU ZA CHAMA KUFUNGUA MATAWI

SACCOS iliyosajiliwa haitapaswa kufungua tawi kwa ajili ya kupanua shughuli zake, isipokuwa kama imepewa leseni na kwa ridhaa ya maandishi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika. SACCOS yenye leseni inayotaka kufungua tawi kwa ajili ya kupanua shughuli zake itapaswa kutuma maombi ya maandishi kwa Mrajis ili aridhie. Maombi yatakayotumwa yanapaswa kuainisha taarifa zifuatazo:-

i. Eneo linalopendekezwa kwa ajili ya kufungua tawi;
ii. Lengo na madhumuni ya kufungua tawi jipya;
iii. Matokeo ya kifedha yatakayotokana na kufungua tawi, ikiwa ni pamoja na mapato yatakayozalishwa na gharama zitakazohusika;
iv. Maelezo ya namna tawi litakavyopata fedha za kujiendesha ikiwa ni pamoja na nakala ya makubaliano ya upangaji na ugharamiaji;
v. Makisio ya mizania na mapato na matumizi kwa muda wa miaka miwili baada ya kuanza tawi kuanza shughuli zake;
vi. Mapendekezo ya muundowake, majina na wasifu binafsi wa wafanyakazi muhimu katika tawi; na

vii. Taarifa nyingine kama Tume itakavyoelekeza.

Mrajis hatapaswa kuidhinisha SACCOS yoyote yenye leseni kufungua tawi isipokuwa awe amefanya ukaguzi wa eneo linalofunguliwa tawi ili kujua utayari wa SACCOS kuanza shughuli zake. Mrajis anaweza kutoa miongozo itakayoeleza mambo ya kuzingatia katika kufungua na kupanua matawi ya SACCOS yenye leseni

### *5.1 KUBADILISHA ENEO LA BIASHARA*

SACCOS yenye Leseni haitatakiwa kubadili eneo la biashara pasipo ridhaa ya Mrajis. SACCOS itakayohitaji kubadilisha eneo la biashara itapaswa kutuma maombi kwa Mrajis ili kupata idhini. Aidha maombi hayo yataambatishwa na taarifa zifuatazo;-

i. Sababu za kubadilisha eneo
ii. Mpango wa ulipaji madeni.
iii. Maandalizi yaliyokamilika ya eneo jipya la biashara.
iv. taarifa zozote zile ambazo Mrajisi atakavyoelekeza

### *5.2 SHUGHULI ZA UWAKALA AU HUDUMA NYINGINEZO*

SACCOS yenye leseni haitaruhusiwa kufungua au kuendesha shughuli za uwakala na kutoa huduma nyinginenezo bila idhini ya Mrajis. SACCOS yenye leseni ambayo inataka kufungua au kuendesha uwakala au milango ya huduma itapaswa, kuwasilisha maombi ya maandishi kwa Mrajis ili kupata idhini yake na maombi hayo yataambatishwa na yafuatayo:-

i. Nakala ya mkataba wa uwakala kati ya wahusika;
ii. Vielelezo vya usalama na eneo lililopo kwa ajili ya kutoa bidhaa na huduma za SACCOS yenye leseni; na
iii. Taarifa nyingine kama Tume itakavyoelekeza.

SACCOS yenye leseni haitapaswa kuwa wakala wa taasisi yoyote ya fedha bila idhini ya maandishi ya Mrajis.

### *5.3 MAHITAJI YA UENDESHAJI WA CHAMA*

SACCOS yenye leseni itapaswa kufanya mambo yafuatayo:-

i. Kuandaa taarifa ya fedha ya mwezi, taarifa ya mikopo iliyocheleweshwa na umri wa mikopo, Akiba, mkopo na taarifa ya uwekezaji;

ii. Kutenga asilimia kumi na tano (15%) ya mali zinazoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ya Akiba na amana kwa ajili ya mahitaji ya ukwasi.
iii. Kufanya uchambuzi wa ukwasi kwa kila mwezi, robo mwaka na mwaka kwa kuzingatia matukio yanayoweza kuathiri ukwasi; na
iv. Kufanya uchambuzi wa mali na dhima kwa kila robo mwaka kwa kuzingatia menejimenti ya kiwango cha riba hatarishi na muundo wa mizania
v. Kuleta maombi ya kuhuwisha kwa leseni ya usajili kwa kila mwaka ikiambatana na ada kulingana na maelekezo ya Mrajis

Wajumbe wa Bodi ya SACCOS yenye leseni watapaswa kukutana angalau mara moja kwa kila robo mwaka.

## 6.0 MIKOPO SHIRIKISHI (*Loan participation*)

SACCOS yenye leseni inaweza kukopa au kukopesha SACCOS nyingine kwa ajili ya kupata fedha za kukidhi mahitaji ya ukwasi ikizingatiwa kuwa:-

i. SACCOS yenye leseni inayokopa haitapaswa kukopa kiwango kinachozidi ukomo wa mikopo kutoka nje ulioainishwa katika Kanuni za SACCOS;
ii. Wajumbe wa Bodi ya SACCOS yenye leseni watapaswa kuidhinisha ukopaji au ukopeshaji kwa SACCOS nyingine
iii. Endapo SACCOS yenye leseni inakopesha SACCOS nyingine, itapaswa kumiliki angalau asilimia kumi ya kiasi cha mkopo husika; na
iv. Vigezo na masharti ya kukopa au kukopesha yatapaswa kuthibitishwa na mkataba uliosainiwa kati au miomgoni mwa SACCOS zinazoshirikiana na mkataba huo utapaswa kuidhinishwa na Mrajis

Endapo, SACCOS yenye leseni siyo mkopeshaji wa awali itapaswa kushiriki tu kwenye mikopo ambayo inaweza kutoa na SACCOS hiyo itapaswa:-

i. Kuwa na Sera ambayo inaainisha viwango vya udhamini wa mikopo kabla ya kuingia katika makubaliano ya mikopo shirikishi;
ii. Kushiriki tu katika mikopo inayotolewa kwa wanachama au wanachama wa SACCOS nyingine inayoshiriki;
iii. Kubaki na nakala halisi au nakala ya makubaliano ya maandishi ya kushirikiana na jedwali la aina ya mikopo itakayohusika katika makubaliano; na

iv. Kupata idhini ya wajumbe wa Bodi kwa ajili ya kutoa mkopo.

## 7.0 USIMAMIZI WA KISHERIA

Mrajis anaweza kuiweka SACCOS yenye leseni chini ya usimamizi wa kisheria iwapo Bodi au uongozi wa SACCOS husika:-

i. Kwa makusudi imeshindwa kutii maelekezo yanayotolewa na Mrajis;
ii. Imeacha kufanya shughuli zake za msingi inazopaswa kufanya au haifanyi shughuli hizo kwa maslahi ya wanachama;
iii. Haina uwezo wa kutatua matatizo ya kifedha yanayotishia uhai wa SACCOS; na
iv. Imejihusisha katika shughuli za kifedha zisizo halali zinazosababisha kushuka kwa mtaji kwa kiwango cha juu.

Aidha Mrajis anaweza kuiweka SACCOS yenye leseni chini ya usimamizi wa kisheria iwapo hali yake ya kifedha na maslahi ya wanachama wake yanaathirika kiasi kwamba:-

i. Haina uwezo wa kukidhi mahitaji ya wanahisa wake,wawekaji wa Akiba na Amana au wadeni;
ii. Mtaji msingi wake upo chini ya asilimia mbili (2%) ya mali zote na umekuwa ukipungua kwa kipindi cha miezi kumi na mbili; na
iii. Mtaji tete wake upo chini ya asilimia tatu (3%) ya mali zote na umekuwa ukipungua kwa kipindi cha miezi kumi na mbili.

Hata hivyo, matumizi yote yanayohusiana na usimamizi wa kisheria ikiwa ni pamoja na mshahara wa Meneja Msimamizi yatapaswa kuidhinishwa na Mrajis na yanaweza kulipwa kutokana na bajeti ya SACCOS.

Mtu yeyote hatateuliwa kuwa Meneja Msimamizi wa SACCOS yenye leseni iwapo mtu huyo ni mwanachama, mdeni au mtu mwenye uhusiano wa karibu.

Kuanzia muda ambao usimamizi wa kisheria umewekwa, mambo yafuatayo yatazingatiwa:-

i. Meneja msimamizi atafanya kazi kwa maslahi ya wanachama na usalama wa fedha zao;
ii. Hakuna mali au dhamana yoyote ya SACCOS itakayozuiwa kwa dai lolote isipokuwa dai lilowekwa na Mrajis kwa kipindi ambacho Meneja Msimamizi anasimamia SACCOS husika; na

iii. Uhamishaji wa mali zozote za SACCOS uliofanywa ndani ya mwaka mmoja kabla ya SACCOS kuwekwa chini ya usimamizi wa kisheria utasitishwa na mali hizo zitapaswa kukabidhiwa kwa Mrajis.

## 8.0 UDHIBITI WA MENEJA MSIMAMIZI

Kwa madhumuni ya kudhibiti usimamizi wa kisheria, Mrajis anaweza:-

i. Kumwelekeza meneja msimamizi namna ya kupima mafanikio ya usimamizi wa kisheria;
ii. Kufanya marekebisho ya mpango kazi wa utekelezaji wa meneja msimamizi kabla au wakati wa utekelezaji
iii. Kuomba na kupokea taarifa kutoka kwa meneja msimamizi kuhusu maendeleo ya SACCOS yaliyopatikana tangu kuwasilishwa kwa taarifa ya mwisho;
iv. Kuongeza muda wa awali wa usimamizi wa kisheria;
v. Kumbadilisha meneja msimamizi iwapo hajaridhika na utendaji wake au matokeo ya usimamizi wake; au
vi. Kusitisha usimamizi wa kisheria au kufuta leseni ya SACCOS na kuanza taratibu za ufilisi

### *8.1 MAJUKUMU NA MAMLAKA YA MENEJA MSIMAMIZI*

Katika kutekeleza majukumu yake ya kiutendaji, meneja msimamizi atapaswa muda wote kuwa na na jukumu la kutunza mali za SACCOS na kuirudisha SACCOS katika hali nzuri kifedha. Aidha, atatekeleza mamlaka yake kwa mujibu wa vigezo na masharti yatakayotolewa na Mrajis.

## 9.0 KUSITISHWA KWA MALIPO YA FIDIA YA USIMAMIZI WA KISHERIA

Mrajis wa Vyama vya Ushirika atasitisha usimamizi wa kisheria baada ya mwaka mmoja ikiwa hali ya kifedha na shughuli za SACCOS imeimarika. Hata hivyo, kwa kuzingatia Kanuni za SACCOS, Mrajis anaweza kuongeza mwaka mmoja wa ziada iwapo hali ya kifedha na uendeshaji wa shughuli za SACCOS haujaimarika.

Baada ya kusitisha usimamizi wa kisheria, mabadiliko yote yaliyofanywa katika sera, taratibu na uongozi katika kipindi cha usimamizi yataendelea kuwa halali isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Mrajis.

Meneja msimamizi hatapaswa kuwajibika kwa hasara zinazotokana na shughuli za kawaida za chama, Aidha, Meneja Msimamizi atawajibika kwa hasara yoyote ya SACCOS itakayotokana na uzembe wake.

## 10. HITIMISHO

Endapo mwongozo huu utazingatiwa katika utoaji wa leseni na usimamizi wa SACCOS kubwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za SACCOS, utasaidia katika ufumbuzi wa hatari zitakazojitokeza kwenye soko la fedha nchini ili kukabiliana na ushindani uliopo. Aidha, SACCOS hizi zinatarajiwa kutoa huduma bora zenye kukidhi mahitaji ya wanachama wake kiuchumi na kijamii kwa azma ya kupunguza umaskini, kuwa endelevu na kujenga Imani kwa wanachama. Ofisi ya Mrajis itahakikisha kuwa taratibu za usimamizi na uendeshaji wa SACCOS zinafuatwa ili kupata matokeo chanya kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo.

*VIAMBATISHO:*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA**

**FOMU Na. 1**

*(Chini ya Kanuni ya 14(2)(b))*

**FOMU YA MAOMBI YA LESENI**

1. Jina la SACCOS:........................................................................................................

   Namba ya Usajili...............................Tarehe ya usajili..................................................

2. Mahali ilipo Ofisi iliyosajiliwa:...............................................................................

3. Anwani ya mahali ilipo Ofisi ya Makao Makuu: L.R. Na................................................

   Mtaa:.........................................................................................................................

   Jengo:........................................................................................................................

4. Anwani ya posta...............................Geresho la Posta.................................................

Namba ya Simu..............................................................................................................

Barua Pepe......................................................................................................................

5. Majina ya maeneo ya biashara katika Tanzania na idadi ya miaka ambayo kila eneo lilianzishwa na kufanya biashara.............................................................................................

| *Na.* | *Jina la Tawi* | *Mwaka wa Kuanzishwa* | *Idadi ya miaka ya kufanya kazi* |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |

NB: Ambatisha pamoja na maombi haya orodha ya maeneo mengine ya biashara. Ainisha majina ya maeneo ya biashara aina kama ni ya setelaiti, Kitengo Tembezi, ATM au Kituo cha Mauzo.

6. Majina ya zamani, kama yapo, ambayo yalitumiwa na SACCOS:

| *Na.* | *Jina* | *Mwaka wa Kutumika* | |
|---|---|---|---|
| | | *Kutoka* | *Hadi* |
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |

7. Maelezo ya mtaji:

(a). Idadi na thamani ya hisa zilizolipiwa.............................................................................

(b). Mtaji Tete..................................................................................................................

8. Taarifa za Maafisa:

(a). Wajumbe wa Bodi:

| *Na.* | *Majina* | *Tarehe ya Kuzaliwa* | *Elimu/Weledi* | | *Tarehe ya Kuchaguliwa* | *Nafasi nyingine anazoshikilia* |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | *Kiwango* | *Mwaka wa kuipata* | | |
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |

(b). Watendaji Waandamizi:

| *Na.* | *Majina* | *Cheo* | *Tarehe ya Kuzaliwa* | *Elimu/Weledi* | | *Tarehe ya Kuajiriwa* | *Ajira ya Kabla* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Kiwango* | *Mwaka wa kuipata* | | |
| 1. | | | | | | | |
| 2. | | | | | | | |
| 3. | | | | | | | |
| 4. | | | | | | | |
| 5. | | | | | | | |
| 6. | | | | | | | |
| 7. | | | | | | | |

9. Majina na Anwani za Benki:

| *Na.* | *Jina la Benki* | *Anwani* | *Namba ya Simu* | *Barua Pepe* |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | | | | |
| **2.** | | | | |
| **3.** | | | | |
| **4.** | | | | |
| **5.** | | | | |

10. SACCOS ilishawahi kuwekwa chini ya uangalizi au kufanya maafikiano au mapatano na wadai wake au vinginevyo kushindwa kulipa wadai wake?................................. ikiwa ndiyo, toa maelezo yake ..................................................

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA**

**FOMU YA LESENI**

**FOMU Na. 2**

*(Chini ya Kanuni ya 16(1))*

Namba ya Leseni...............................................

LESENI hii imetolewa kwa.....................................................yenye namba ya usajili.............................. na anwani........................................ na inaidhinisha SACCOS hii kutoa bidhaa na huduma zinazoruhusiwa kutolewa na SACCOS iliyo iliyosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***LESENI hii imetolewa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zilizotolewa chini yake na kwa masharti yoyote yaliyotolewa hapa.***

Masharti

1. ........................................................................................................................
2. ........................................................................................................................
3. ........................................................................................................................
4. ........................................................................................................................

LESENI hii inahusu kipindi cha kuanzia siku ya tarehe.............mwezi wa ......................mwaka ................hadi siku ya tarehe............mwezi wa .....................mwaka ................kwa ofisi ya makao makuu ya SACCOS na maeneo ya biashara mengine ambayo yameambatishwa na maombi ya LESENI hii.

Tume inaweza kwa wakati wowote kufuta, kuibadilisha au kuiwekea zuio LESENI hii au kubadilisha vigezo na au masharti ya kutolewa kwake.

Imetolewa chini ya Lakiri ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Siku ya tarehe...............mwezi wa ......................................mwaka...................

..............................................................................

**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

FOMU Na. 3

**Fomu ya Tamko la Mali**

*(Chini ya Kanuni ya 131)*

**TAMKO LA MASLAHI, MALI NA DHIMA KWA VIONGOZI WA SACCOS**

| | |
|---|---|
| **ZINGATIA:** | **WANACHAMA WANASHAURIWA KUSOMA KWA UMAKINI NOTISI/TAARIFA/MAANDISHI KWA AJILI YA UKAMILISHAJI WA TAMKO LA MALI. FOMU HII ITAPASWA KUJAZWA NA VIONGOZI WOTE WA USHIRIKA (WAJUMBE WA BODI, WAJUMBE WA KAMATI NA WATUMISHI WOTE WA NGAZI YA JUU KATIKA MENEJIMENTI YA SACCOS** |

**Hali ya Tamko:**

*(Weka vema kwenye kisanduku husika)*

1. Jina la Ukoo la Mtoa Tamko..............................................................................................

*(Kwa herufi kubwa)*

Majina mengine:

......................................................................................................................

2. Tarehe ya kuzaliwa:
......................................................................................................................

3. Mahali pa kuzaliwa:
......................................................................................................................

*(Kijiji, Kata na Wilaya)*

4. Hali ya ndoa: ...................................................................................................

5. Uraia: ..........................................................................................

6. Anwani S.L.P .....................................................

a) Mahali anapoishi: ...............................................

b) Simu:.............................................................................

7. Taarifa Binafsi

*(a)* Cheo/Nafasi/Wadhifa: ..........................................................................................

(b) Tarehe ya uteuzi wa cheo cha sasa:.............................................................................

(c) Jina la Mwajiri: .......................................................................................................

(d) Hali ya ajira (mkataba, kudumu, muda n.k.)..................................................

(e) Mshahara kwa mwaka:..............................................................................................

(f) Posho kwa mwaka (makisio) ......................................................................................

(g) Vyanzo vingine vya mapato:.......................................................................................

**8. TAARIFA ZA MAPATO:**

(a) Fedha taslimu zilizopo Benki au Taasisi nyingine za fedha zilizopo Tanzania

.......................................................................................................................

*(Taja eneo ilipo benki/taasisi ya fedha, jina/majina ya wenye akaunti, namba ya akaunti, aina ya akaunti)*

Jina la Benki/ Taasisi

na.......................................................................................

Mahali...................................................................................

Jina/majina ya Wamiliki wa Akaunti.......................Aina ya akaunti

akaunti.namba.............................................................................

(b) Fedha zilizoko kwenye benki au Taasisi za Fedha zilizopo nje ya Tanzania

*(Toa maelezo kama yaliyopo hapo juu (a) na maelezo ya nchi husika).*

Jina la Benki/Taasisi na Mahali

Jina/Majina ya Wamiliki wa akaunti ..........................Aina ya akaunti na namba

yake.................................................................................................

(c) thamani ya dhamana Uwekezaji ................................................................

*(Toa maelezo na anuani za benki/kampuni na kiasi)*

(d) Kiasi cha fedha unachomdai na

mdeni/mwiwa/mdaiwa.......................................................

(e) Toa maelezo ya deni/madeni:

..................................................................................

**9. MAELEZO YA MALI:**

**(a) Ardhi ambayo haijaendelezwa.**

(i) Mahali ilipo nchini

Tanzania...........................................................................

*Kijiji..................................., Kata............................., Wilaya......................*

*Thamani ya sasa katika kuinunua/kuipata....................................................*

*Namba ya Kitalu................ na Kiwanja..................* (ii) Mahali ilipo nje ya Tanzania

.........................................................................

(iii) Eleza namna ardhi ilivyopatikana na vyanzo vya mapato endapo

imenunuliwa..................................................................................

**(b) Ardhi (jengo/nyumba) iliyoendelezwa**

(i) Mahali ilipo nchini Tanzania.............................................

*Kijiji........................., Kata................/........, Wilaya....................,*

*Namba ya Kitalu................, Kiwanja ...............*

(ii) Mahali nje ya

Tanzania.......................................................................................

(iii) Taja chanzo cha fedha, kama nyumba/jengo ulilinunuwa au

kulijenga......................................

(iv) Taja mapato kwa mwaka kama nyumba/jengo ni kwa ajili ya Biashara

..........................................................................................................

**(c) Shamba**

(i) Mahali lilipo nchini Tanzania

*Kijiji ........................................................ Kata, ......................Wilaya.............*

*Thamani ya Soko ..................................................*

*Namba ya shamba ..................tarehe ya kununua/kumiliki .....................*

(ii) Mahali lilipo nje ya Tanzania

.....................................................................................................

(iii) Elezea jinsi kila shamba lilivyopatikana, kama lilinuliwa eleza chanzo fedha

..............................

(v) Eleza mapato kwa mwaka yanayotokana na shughuli za kila shamba lililotajwa hapo

juu...................

**(d) Gari/Magari**

(i) Aina na Namba ya Usajili:

.................................................................................

(ii) Thamani na tarehe wakati wa

kununua.................................................................................

(iii)Thamani ya Soko kwa sasa (makisio)

.................................................................................

(iv) Eleza jinsi kila gari lilivyopatikana/nunuliwa na chanzo cha fedha kama

lilinuliwa...........................

(v) Eleza jinsi kila gari linavyotumika (Binafsi au Biashara)...................

Kama linatumika kibiashara eleza mapato kwa mwaka.........................

**(e) Hisa katika Biashara/Kampuni ndani na nje ya Tanzania**

*Jina na Namba ya Anuani ya Biashara/Kampuni na hali ya hisa za Biashara*

(ii) Eleza jinsi hisa zilivyopatikana..............................................................,

kama zilinunuliwa elezea chanzo cha fedha..................................................

(iii) Eleza mapato kwa mwaka yanayotokana na biashara ya hapo juu........................

(f) **Mali nyingine .**

(i) Thamani ya kifaa wakati wa kununuliwa:......................................................

(ii) Na tarehe kiliponunuliwa..........................................................................

(iii) Thamani ya Soko kwa sasa (makadirio)..................................................

(a) **Maslahi/Nafasi au Cheo:** Je wewe ni kiongozi katika nafasi yoyote ya kuchaguliwa au kuteuliwa kisiasa? (angalia kifungu cha 132 (4) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika), Kama NDIYO, taja nafasi na miaka umekuwa katika cheo hicho:

..........................................................................................................

..........................................................................................................

Mimi, .......................................................................................................... nikiwa nimechaguliwa/ kuteuliwa na kuapishwa/kukabidhiwa ofisi ya ..........................................................................................................

tarehe ........................ siku ya........................ 20........ natamka kwa uaminifu na dhati kuwa mpaka kufikia siku ya leo namiliki and kudaiwa mali na madeni zilizotajwa hapo juu

Natoa tamko hili kwa uaminifu nikiamini kuwa la kweli na kwa mujibu wa Sheria ya Viapo na Matamko ya Kisheria [Sura ya 34 ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002].

**TAMKO**

Tamko hili limetolewa na kusajiliwa/kuandikishwa kwenye.............................

Kutoka kwa ..............................................................................................

Ambaye namfahamu/ametambulishwa kwangu

Kutoka kwa..............................................................................................

Ambaye namfahamu binafsi

leo .....................siku ya.................20...............................................

} **MTOA**

**MBELE YA:**

Saini: ..........................................................................

Cheo: ..........................................................................

Anwani: ......................................................................

...................................................................................

...................................................................................

...................................................................................

*(Tamko hili lazima lifanyike mbele ya Kamishina wa Viapo au Mthibitishaji wa Umma)*

KWA: MRAJIS,

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

**KWA MATUMIZI YA OFISI**

1. Tarehe ya Tamko: ...........................................................................

2. Tarehe ya kupokea Tamko: .........................................................

3. Hatua iliyochukuliwa......................................................

(a) Hati ya kukiri iliyotolewa:...................................................

(b) Kuwekwa kwenye jalada: ..........................................................

(c) Kutumwa kwa ajili ya uhakiki/ufafanuzi:

(d) Maoni:...................................................................

Jina la Afisa aliyepokea:..........................................

Cheo:..............................................................

Saini:.......................................................